

**SHULE YA UPILI YA GATITU
MTIHANI WA KATIKATI YA MUHULA WA KWANZA(2016)**

JINA.....DARASA.....NAMB.....

SHAIRI

Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali

1. 1. Wenye vyao watubana, twaumia maskini,
La kufanyiza hatuna, hali zetu taabani,
Kwa sasa kilo ya dona, bei mia ishirini,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.
2. Washindana matajiri, kwa bei siyo utani,
Na pigo kwa mafakiri, tunao hali ya chini,
Wazeni kutafakari, wanyonge tu madhilani,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.
3. Limekuwa kubwa zogo, hakwendeki madukani,
Fungu moja la muhogo, sasa shilingi miteni,
Huo mkubwa mzigo, waelemea vichwani,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.
4. Si hichi wala si kile, hakuna cha afueni,
Bei imekuwa ndwele, wenye macho lioneni,
Ukiutaka mchele, pesa jaza mfukoni,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.
5. Waliko hao samaki, huko ndiko uchawini,
Wachuuzi hawacheki, zimewatoka huzuni,
Vibuwa havishikiki, kimoja kwa hamsini,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.
6. Maisha yetu viumbe, yamekuwa hilakini,
Wenye vyao kila pembe, wametukaa shingoni,
Nyama ya mbuzi na ng'ombe, sasa hali maskini,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.
7. Maji yamezidi unga, kwa lodi wa darajani,
Kajitolea muhanga, kwa bei hawezekani,
Mvao wake wa kanga, ni shilingi elifeni,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

Maswali

(a) Fafanua toni ya shairi hili.

(alama 2)

(b) Jadili dhamira ya nafsi neni. (alama 2)

.....
.....

(c) Andika ubeti wa *sita* kwa lugha nathari. (alama 4)

.....
.....
.....

(d) Fafanua kwa kutoa mfano, mbinu moja aliyotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika shairi hili. (alama 2)

.....
.....

(e) Taja na ueleze bahari mbili za shairi hili ukizingatia: (alama 2)

(i) vipande:.....

(ii) Vina:.....

(f) Taja na ufafanua tamathali za usemi zilizotumika katika shairi. (Alama 2)

.....
.....
.....

(g) Ujumbe unaowasilishwa katika shairi hili una hadhira lengwa tatu. Zitaje na utoe mifano. (alama 6)

.....
.....
.....
.....

KIDAGAA KIMEMWOZEA

2. "Aliwaonea gere wanawake wengine katika eneo la Sokomoko waliovaa rinda moja....."

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)

.....

.....

.....

.....

b) Eleza sifa na umuhimu wa anayemfanya mrejelewa kuwaonea wanawake wengine gere (alama 10)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

c) Jadili maudhui matatu yanayodokezwa katika dondoo hili (alama 6)

.....

.....

.....

.....

.....
.....
.....
.....
.....

SARUFI

1. Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mstari chini. (Alama 2)

a. Ubaguzi wa kijinsia umekashifiwa na viongozi wenye msimamo dhabiti.

.....

b. Wao walirauka asubuhi na mapema kwenda kumsaidia nyany yao.

.....

2. Bainisha aina za vishazi katika sentensi hizi (Alama 2)

Wakati alipokuwa mhubiri aliwahubiria wengi.

.....

Mwanariadha aliyefanya mazoezi uwanjani alishinda katika mchuano huo.

.....

3. Fafanua mofimu katika neno hili. (Alama 3)

Msiwatenganishe

.....

.....

4. Changanua sentensi ukitumia njia ya matawi. (Alama 3)

Mtoto aliyeokolewa juzi hajapatana na jamii yake.

.....
.....
.....
.....
.....

DAMU NYEUSI

Huku ukitoa mifano maridhawa, onyesha jinsi wanawake wamesawiriwa katika Diwani ya Damu Nyeusi kwa kurejelea hadithi zozote *tatu*.

AU

Uozo wa jamii umesheheni katika jamii.Fafanua ukirejelea hadithi zifuatazo:**Samaki wa nchi za joto,Damu nyeusi,Glasi ya mwisho makaburini**

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....